MUHTASARI WA TAARIFA YA MPANGO MKAKATI WA MAZINGIRA WA WILAYA YA MAFIA

Kilindoni, Mafia District © H. Sosovele, 2008

Mafia Airstrip, Boubacar Thiam, 2008

Umeandaliwa kwa pamoja

Na International Resource Group (IRG), Washington, DC

Na Taasisi ya Kutathmini Rasilimali, Chuo Kikuu, Dar es Salaam,

Na International Union for the Conservation of Nature (IUCN), Ofisi ya Dar es Salaam

Kwa niaba ya Millennium Challenge Account-Tanzania, Dar es Salaam

November 25, 2008

MUHTASARI WA TAARIFA YA MPANGO MKAKATI WA MAZINGIRA KWA WILAYA YA MAFIA

UTANGULIZI

Hii ni taarifa ya utafiti uliofanyika Kisiwani Mafia kuanzia Mwezi June 2008 ambapo watafiti walianza na udadizi wa kwanza. Utafiti ulihusha njia mbalimbali iliwa ni pamoja na kutembelea maeneo mbali mbali na kuhojiana na wananchi kwa undani ulianza mwezi July 2008 na kukamilika mwezi Agasti 2008 mwishoni. Watafiti walikamilisha utafiti wao kwa kuhojiana na watendaji na baadhi ya viongozi wa Serikali kuu, Wilayani, kuzungumza na wananchi katika maeneo yao kwa mikutano ya Kata ambayo ilihudhuriwa na wanavijiji na viongozi wao kutoka kata hizo. Vile vile watafiti walizungumza na kuhojiana na viongozi Wilayani na Wizara husika Dar es Salaam na Kibaha, Mkoa wa Pwani ili kupata maoni na mapendekezo yao.

Madhumuni ya Utafiti huu wa Mkakati wa mazingira ni kuweza kubainisha matatizo ya mazingira na kijamii yanayoweza kutokea kutokana na mipango mbalimbali ya maendeleo wilayani Mafia ikiwa ni pamoja na kuboresha uwanja wa ndege wa Mafia. Utafiti huu unakusudia kupendekeza utayarishaji wa mipango ya mendeleo ya mfupi na muda mrefu kwa ajili ya Kisiwa cha Mafia ambayo itaisaidia MCC na Serikali ya Tanzania kuweka mipango ya kipaumbele katika uwekezaji ambao utaibuliwa na uboreshaji na ujenzi wa uwanja wa ndege wa Mafia ili kuhakikisha kuwa shughuli hizo zinakuwa endelevu.

Kwa sasa, Kisiwa cha Mafia ni muhimu sana kwa sekta ya utalii. Bila ya kuzingatia uwezo na uhimilivu wa kisiwa katika nyanja mbalimbali, maendeleo ya utalii na mengineyo yanaweza kuleta athari mbaya katika mazingira na raslimali zake ambazo zinategemewa na sekta hiyo.

Utafiti wa kuandika huu Mpango Mkakati umefanywa na Taasisi ya Kutathimini Raslimali ikishirikiana na IRG ya Marekani (USA) kwa niaba ya Wizara ya Miundombinu ikishirikiana na Millenium Challenge Compact na Millenium Challenge Account (MCC/MCA-T) ambao ndio Wadau wa mpango huu.

Rais George W. Bush wa Marekani na Rais Jakaya Kikwete wa Tanzania walitia saiani mweazi Februari 2008, makubaliano ya msada wa Dola za Marekani Millioni 698. 1 kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Changaamoto ya Milenia. Lengo la Mpango wa Changamoto ya Mileai ni kupnguza umasikini Tanzania, kuamusha ukuaji uchumi, kuongeza kipato ngazi ya kaya na kuongeza ubora wa maisha kupitia uboreshaji wa miundo mbinu kama usambazaji wa maji, barabara na nishati. Uboreshaji wa Uwanja wa ndege wa Mafia ni mpango mmojawapo kati ya hiyo.

Kwa muuda mrefu njia pekke ya usafiri kwenda Mafia ni usafiri wa baharini, ambao si bora na salama. Wilaya ya Mafia haifikiki kiurahisi na hali hii imedunisha maendeleo wilyani humo na kuwakatisha tamaa wataalam wengi ambao wamepangiwa kufanya kazi huko. Hali hii imedumaza maendeleo ya Mafia. Ubireshaji wa uwanja wa ndege unaweza kuamsha na kuchochea kukua kwa shughuli mbali mbali za uchumi, ambazi zinaweza kuathir mazingira na hali ya kijamii Mafia. Ni kwa kutambua hali hii, Wizara ya Miundo Mbinu kwa kushirikiana na Ofisi ya Akaunti ya Changamoto ya Milenia Tanzania, wameamua kufanya tathmini ya Mkakati ya Mazingira ili kubaini matatizo ya kisera na program yanayoweza kujitokeza na kutoa mapendekezo ya namna ya kukabiliana na changamoto hizo na kuboresh faid zitokanazo na utakelezaji wa miradd mbalimbali Wilayani Mafia. Muhtasri huu unatokana na taarifa ndefu ambayo inaainisha masuala mbali mbali ya kuzingatiwa endapo miradi na shughuli mbali mbali za kiuchumi zitatekelezwa Mafia.

HISTORIA KWA UFUPI- WILAYA YA MAFIA

Mafia ni mojawapo ya Wilaya 6 za Mkoa wa Pwani ambao makao yake makuu ni Kibaha. Uchumi wa Mafia unategemea mazao ya kilimo kama vile minazi, korosho, mpunga, mboga na viaza vitamu pamoja na mifugo. Uvuvi ni sehemu kubwa ya shughuli za uchumi katika Wilaya ya Mafia kwa ujumla. Kilimo hakifanyiki sana katika visiwa vidogo vya Mafia kwa kuwa vingine havina ardhi ya inayofaa kwa kilimo. Wananchi wengi wa Mafia wanakipato cha chini, na wanaofuata sana utamaduni wa Pwani wenye utando wa mshikamano mzito wa familia na maadili ya dini.

Mafia ina utajiri mkubwa wa mazao ya bahari ya Hindi ikiwa ni pamoja na zaidi ya aina 350 za samaki pamoja na kamba na pweza. Upungufu wa samaki katika maeneo mengine ya bahari nchini Tanzania umefanya wavuvi kuhamia Mafia kwa uvuvi na kuendeleza uvuvi haramu. Hii imekuwa ikisababisha msuguano wa mara kwa mara kati ya wavuvi na kati yao na serikali kutokana na matumizi ya njia haramu za uvuvi, kumalizaika kwa samaki na uharibifu wa mazingira ya bahari. Mwaka 1995 Hifadhi ya Bahari ya Mafia ilianzishwa ili kuendeleza uhifadhi wa viumbe mbalimbali vya bahari na mazingira yake. Hifadhi hiyo ni ya matumizi mbali mbali pamoja na makazi ya zaidi ya asilimia 50 ya tu wa Mafia ambao wanaishi na kufanya shughuli zao ndani ya hifadhi.

Mafia inautajiri mkubwa. Pamoja na hifadhi ya bahari na viumbe wake maarufu kama vile Potwe, kuna Popo na baadhi ya aina ya vyura na mijusi ambao hawapatikani maeneo mengine yoyote duniani. Kuna mapango ya asili, magofu yenye historia ya kale na utamaduni ambao haupatikani maeneo mengine yoyote nje ya Mafia. Hivyo Mafia inakuwa ni sehemu mojawapo kuu ya Utalii Tanzania. Utalii huu ukiboreshwa utakuwa kichocheo kizuri cha kuinua kipato cha wananchi, kuboresha maendeleo na kuondoa umasikini. Usafiri wa anga kwa Mafia umeongezeka kuanzaia mwaka 1999 na unatarajiwia kuongezeka zaidi kufikia wasafiri 180,000 na mizigo kilo millioni 1 and laki nne kufikia mwaka 2030. Mafia pia imeanza kuwa muhimu katila utafautaji wa nishati ya gesi pale Ndagoni.

Mipango mbalimbali ya ewekezaji Mwafia inaweza kuleta madhara na hasara katika uchumi wa wilaya, wananchi na tamaduni zao, mazingira na mahusiano ya kijamii. Uharibifu wa mazingira unaweza kundelea hat pasipo kuboresha uwanja wa ndege japo kuwa kiwango na kasi ya uharibifu huo vinaweza kuwa kidogo. Hata hivyo uhaibifu huo na msukumo mkubwa katika matumizi ya rasilimali, vinatokea pasipo kuwepo na uwezo wa kutosha wa Wilaya kupanga na kusimamia matumizi ya rasilimali.

MAKUSUDI YA TATHMINI YA MKAKATI WA MAZINGIRA KWA MAFIA

Wizara ya Maendeleo ya Miundombinu kwa kushirikiana na Akaunti ya Changamoto ya Milenia Tanzania waleannzisha ufaiti na tathimini hii ya Mkakati ya Mazingira kwa Mafia. Tathmini za ain hii ni nyenzo za kuwezesha kuoanisha masuala ya mazingira katika mipango na mikakati mbalimbali Katia kiwango cha sera na maamuzi ya kisiasa. Masual ya mazingira yanaingizwa Mwanza kabisa katika mipango kabla maamuzi ya kisiasa hayajachukuliwa. Pia tathmini hizo zinatoa fursa kwa viongozi kutafakari juu ya sera na porgramu mbadala zanazohifadhi mazingira na kufanikisha malengo yale yale ya maendeleo.

Tathmini hii imetumia njia nyingi mbalimbali za kuwahusisha wadau ikiwa ni pamoja na mikutano ya vikundi maalumu vya wataalamu, vatu maarufu, mahojiano na mti mmoja mmoja, kutembelea sehemu mbalimbali Mafia, Kibaha, Rufiji, Zanzíbar and Kilwa kuona na kuongega na wadau mbalimbali juu ya mipnago ya maendeleo kwa Mafia na jinsi inavyoweza kuathiri shughuli zao katika maneno yao. Pia watafaikti wameongea na viobgozi mbalimbali wa wilaya, wizara na

taaisisi za umma na binafsi ili kupata maoni yao. Dhana ya ushirikishwaji ulzingatiwa katuka kila hatua ya tahtmini hii.

Tathmini hii imeongozwa na Sheria ya Mazingira Na 20 ya 2004 na Muongozo kutoka Changamoto ya Milenio juu ya thathmini za aina hii na músala ya mazingira. Sheria ya Mazingira ya Tanzania inatoa mwongozo juu ya maeneo ambayo yanatakiwa kufanyiwa Tathmini ya Mkakati ya Mazingira. Maeneo hayo ni sera, mipango, programu, sheria na mikataba ya kibiashara. Uboreshaji wa uwanja wa ndege wa Mafia ni Mkakati ambao unaweza kusababisha mabadiliko makubwa ya kijamii, kisera, kiuchuni na kimazingira hivyo imekuwa lazima tathmini hii kufanyika na kutoa ushauri wa mambo ya kuzingatia.

ATHARI ZA MIPANGO YA MAENDELEO NA MIRADI MBALIMBALI KWA MAFIA

Mipango mbalimbali ya maendeleo inayoweza kutekelezwa kufuatia uboreshaji wa uwanja wa ndege wa Mafia ikiwa ni pamoja na uboreshaji wenyewe wa uwanaja wa ndege inaweza kuleta faida na hasara katika uchumi, masuala ya kijamii, utamaduni na mazingira ya Mafia.

Baadhi ya faida zinazoweza kupatikana kotokana na mipango hiyo kutekelezwa ni pamoja na:

- Kukua kwa nafasi kiuchumi kutokana na kukua kwa utalii na uboreshaji wa miundo mbinu Ambato itarahisisha usafiri na usafirishaji
- Kuongezeka kwa masoko ya mazao yazalishwayo Mafia; mazao ya bahari, mifugo na kilimo
- Kuboreshwa kwa nafasi za kuzalisha mali na kuongeza kipato
- Kuboreshwa kwa huduma za jamii, mawasiliano, benki na jinsi ya kupata taarifa muhimu
- Kuongezeka kwa fursa ya kuongeza na kuboresha utengenezaji na uuzaji wa mazao ya mikono
- Kuongezeka kwa mapato ya Halmashauri na Serikali Kuu
- Kuongezeka kwa nafasi za ushirikishwaji wa wananchi katika maamuzi na utekelezaji miradi ya maendeleo
- Uwezekano wa kuboresha maisha na kuondoa umasikini kutokana na kuboreshwa kwa huduma za jamii, nafasi za kushiriki kiuchumi na kuboreshwa kwa utaalamu na uwezo
- Uwezekano wa kuboreshwa maeneo ya utalii pamoja na magofu ya Kua, vijana kupata ajira na vijiji kupata kipato kutokana na kuanzisha na kushiriki katika shughuli za kitalii.

MATOKEO YENYE KULETA ATHARI

Baadhi ya shughuli za maendeleo Mafia zatakazotokana na uboreshaji wa uwanja wa ndege na mipango mingine ya maendeleo, zinaweza kuleta hasara kama ifuatavyo:

- Uharibifu wa misitu kutokana na ukataji wa miti kwa ajili ya mkaa na ukataji mikoko kwa ajili ya ujenzi na kutengeneza vyombo vya usafiri. Ukataji kufanyika Mafia, Rufiji na Kilwa.
- Utupaji hovyo wa taka ngumu na taka maji na kusababisha uchafuzi wa mazingira, kuathiri maji ya chini ya ardhi, chemchem, bahari na viumbe vyake.
- Uharibifu wa matumbawe kutokana na wingi wa watalii na shughuli zao baharini na katika fukwe na kuharibu maeneo ya mazalia ya Kasa, Potwe, Nguva n.k
- Kumalizika kwa samaki kutokana kuongezeka kwa uvuvi haramu na uharibifu wa mazingira na maliasili za bahari (fukwe, mikoko, maeneo ya mazalia/viota)

- Uwezekano wa ongezeko la watu ambao utaweka shinikizo katika uvunaji kupita kiwango wa maliasili zilizopo, kuongeza mahitaji mbali mbali (huduma za afya, elimu, maji, umeme, ajira).
- Uwezekano wa kuongezeka kwa magonjwa ya kujamiiana (zinaa) pamoja na Ukimwi kutokana na mahusiano ya mapenzi yasiyo salama; kuongezeka kwa magonjwa ya mlipuko (kipindupindu, homa ya uti wa mgongo n.k) kutokana na ongezeko la vatu visiwani Mafia.
- Upungufu wa usalama kutokana na ongezeko la vatu na uwezekano wa Mafia kupata wageni wenye tabia tofauti na weneyeji na kuvuruga umoja, mahusiano yaliyopo sasa Ambato kwa kiwango kikubwa bado ni bora ikilinganishwa na maeneo mengi nchini.
- Kuongezeka kwa ajali barabarani na majini (barabara nzuri, mwendo kasi, kujazana kwa kupita kiasi katika boti).
- Kuharibika kwa magofu na maeneo ya kitalii kutokana na wageni wengi kuyatatembelea (kutasababisha mtikisiko, kukaliwa, kuguswa).
- Kuongezeka kwa msuguano na ugomvi kugombania ardhi na raslimali mbali mbali kati ya wenyeji na asasi za usimamizi wa mazingira na maliasili (MIMP, Halmashauri); kati ya wenyeji na wamiliki wa hoteli na biashara za utalii; baina ya wenyeji kugombania maeneo na baina ya wawekezaji katika sekta ya utalii na biashara husika,
- Kupanda kwa gharama za maisha na bidhaa muhimu kutokana na kuongezeka kwka mahitaji na watumiaji
- Kupoteza haki ya miliki ardhi na raslimali zake na haki ya matumizi ya mapito ya njia kwenda baharini na kwenye fukwe kutokana na uuzaji holela wa ardhi (usiozingatia sheria na haki), fukwe na mazingira yake kwa biashara ya utalii.

MIKAKATI NA MBINU YA KUDHIBITI ATHARI MBAYA

Mpango Mkakati wa Mazingira Mafia umezingatia vigezo mbali mbali katika kushauri mkakati endelevu wa kuboresha mipango mbalimbali ya maendeleo na uboreshaji wa uwanja wa ndege na Utalii Kisiwani Mafia. Ni muhimu kutambua kuwa hakuna mradi wowote wa maendeleo usiokuwa na madhara isipokuwa ni muhimu kuangalia uwezo wa mazingira na raslimali zake na viwango vyake kuhimili vishindo vya maendeleo bila athari kutokea. Uhimilivu wa eneo (carrying capacity) ni uwezo wake wa kubeba mzigo au majukumu yaliyopo na kutoa huduma itakiwayo bila kuathiri utoaji wa huduma husika. Kila kitu au raslimali (watu au maliasili/baoanuai) ina kiwango chake cha mwisho cha uhimilivu kabla hakijateteleka. Wakati mwingine kiwango hicho hufikiwa kwa majadiliano na maamuzi ya ukomo gani utumike wa kufanya shughuli fulani kwa mfano ukomo wa wingi wa watalii kwa msimu ambao hautaathiri utalii na vivutio vyake. Wingi au idadi ya watalii au watu katika eneo moja, majengo katika eneo husika, magali katika eneo husika n.k ni kigezo muhimi kuzingatia ili kuimarisha hifadhi ya mzaingira na kusaidia shughuli husika kuwa endelevu.

Hivyo basi, Tathimini ya Mkakati wa Mazingira kwa Mafia unsahuri kuwa uongozi wa Wilaya ya Mafia na Serikali Kuu budi ufahamu ubaya na uzuri wa maamuzi fulani ili uweze ukafanya maamuzi yanayozingatia vigezo maalum vya kisayansi sio tu matakwa ya hisia au muelekeo binafsi. Kwa mfano, maamuzi ya kuboresha utalii budi yazingatie baadhi ya mambo muhimu yafuatayo:

- Uboreshaji mazingira
- Uwezekano wa kupoteza fedha (Kuwekeza sana katika utalii halafu wasiendelee kuja). Hivyo uamuzi lazima uangalie mengi pamoja na:

Aina ya utalii/watalii wajao na mahitaji yao; idadi na aina ya hotel za kitalii, uwezo wa hoteli na Mafia kwa ujumla katika kukidhi mahitaji ya watalii na wengineo wajao au waliopo wa kuhudumia sekta ya utalii. Maamuzi yafanyikayo yataathiri pia wawekezaji katika utalii.

- Wizara husika (Miundo Mbinu, Mali Asili na Utalii, Maji na miundombinu ya umwagiliaji) kuwa na mikakati endelevu ya uwiano inayokwenda na wakati na inayozingatia vigezo na maangalizo muhimu yatokanayo na ufuatiliaji yakinifu wa mipango na utekelezaji angalifu katika sekta ya utalii, maendeleo jamii na mazingira.

Ushauri ufuatao unatolewa wa kudhibiti athari mbaya:

Mbinu za Kudhibiti Athari

Wizara/Idara Husika (Mdau)	Shughuli za kutekeleza
Wizara ya mali asili na Utalii na Halmashauri ya Mafia	Tayarisha mpango Kamambe wa Utalii ambao utazingatia uwezo himilivu (Carrying capacity) na ustawi wa Kisiwa. Ujio wa watalii na wageni wengine wengi utahamasisha uwekezaji na shughuli nyingine nyingi ambazo zitaleta athari mbaya kwa kisiwa. Bila ya kuwa na mpango kamambe wa uwiano wenye kuzingatia usimamizi bora wa mazingira na wa kisheria Mafia itawea kupata mabadiliko Mabaya ya kudumu yasiyorekebishika. Haya yataweza kuzidisha badala ya kuondoa umasikini na kuboresha uchumi. Mfano, kwa sasa kuna hotel iza kitalii 8 za vyumba jumla ya 78. Kuna mpango wa kujenga 5 zaidi. Abiria wa ndege pamoja na watalii kuanzia 2007 huja 40 kwa siku (13,240 kwa mwaka) Inategemewa wataingia 100 kwa kila saa wastani wa 486 kwa siku (kwa mwaka 177,503), ndege 56 kwa situ (20,611 kwa mwaka ifikapo 2030. Hivyo kutatakiwa kupunguza idadi ya wageni polepole ifikapo 2030 wawe nusu ya wanaokisiwa hapo juu ili kupata mapato ya faida ya muda mrefu bila kuharibu mazingira.
	Kutengeneza mkakati wa kufaidika kwa wananchi wa mafia kutokana na utalii na shughuli nyingine za uwekezaji Mafia. Mfano, ipangwe ni jinsi gani wananchi watafadaidika na utalii (kifedha, ajira na namna nyingine); viwanda, uchimbaji nishati na uwekezaji (ujenzi wa hoteli) na uwekezaji mwingine uingiao Mafia wa watu binafsi, mashirika na miradi ya serikali na yasiyo ya serikali. Kuwe na mikataba na sheria ndogo ndogo ya kulinda kufaidika huko na ufuatiliwe na hatua za kisheria kuchukuliwa inapokiukwa. Wananchi wenye ardhi waelimishwe jinsi ya kuingia ubia wa haki na wawekezaji bila ya kudhulumiwa.
Wizara ya mali asili na Utalii na Halmashauri ya Mafia na Hifadhi ya Bahari (MIMP)	Kuweka kiwango cha idadi ya watalii na mipaka ya matumizi ya maeneo ya nje na ndani ya hifadhi kwa watalii na kuangalia upya sheria ya matumizi ya hifadhi kulingana na wakati na vigezo vya matokeo ya uhifadhi vilivyofikiwa ili kupunguza migogoro na uharibifu wa hifadhi na viumbe vyake.
Halmashauri ya Mafia na Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (Land use Comisión).	Zitengeneze mpango wa matumizi bora ya ardhi Mafia pamoja na kuweka kanda (zones) za aina ya matumizi ardhi (mfano eneo la hoteli na utalii tu, makazi tu, viwanda tu, kilito tu, hifadhi, utalii wa namna fulani tu).
Halmashauri ya Mafia	Kuhakikisha kuwa kila uwekezaji unafanyiwa utafiti wa athari za mazingira na jamii kwa kila mradi uanzishwao kulingana na matakwa ya Sheria ya Mazingira Namba. 191 ya 2004.
	Kuwa na kutekeleza mpange endelevu wa kujenga uwezo kiutendaji wa idara zake katika kutekeleza majuku yahusuyo. Pia, kujenga uwezo wa wananchi ili waweze kujenga kujiajiri (katika utalii, kilimo, ufugaji wa faida, uvuvi, kazi za stadi za mikono na kuuzia watalii na wengineo ndani ya nchi na kusafirisha nje ya nchi).
	Kutekeleza shughuli za maendeleo na kuboresha uchumi ambazo zinatumia teknolojia rafiki na kuwa hazitoi taka hewa, maji na taka ngumu ambazo zina madhara. Na kuona ya kuwa vigezo/viashiria vya nchi na vya kimataifa vya mazingira (maji, hewa, ardhi) na vinginevyo vinazingatiwa.
	Kwa kuzingatia Sera na Mkakati wa Ukimwi kuelimisha wananchi wake

	kwa waume, vijana na wazee kuhusu masuala yote ya Ukimwi na matatizo mengine ya afya yanayoweza kuletwa na uboreshaji wa uwanja wa ndege na utalii na jinsi ya kuepuka.
	Kuhamasisha na kuwaelimisha wananchi wa Mafia jinsi gani wanaweza kutumia fursa zilizopo na zijazo kwa kuwajibika; aina ya uwajibikaji unaotakiwa; kuwawezesha inapobidi ili waweze kutumia fursa hizo. Kufuatilia kuona pale fursa zilipotolewa zimetumika kikamilifu ili kufikia malengo.

NJIA MBADALA ZA KELET MAENDELEO MAFIA

Tathmini ya Mkakakti wa Mazingira kwa Mafia imezingatia njia mbadala za kuele mandeleo Mafia. Hat hivyo inasisitizwa hapa kuwua kila mradi utakaotekelzwa Mafia, uzingatie sheria za mazingira na kufanya tathmini ya athari ya mazingira kwa kila mardi husik kulingana na sheria.

Njia mbadala zailizozingatiwa ni kama zifuatazo.

- **Mbadala wa Mpango wa kutokuwa na Uboreshaji wa |Uwanja wa ndege na utalii ili kuepuka madhara.**

  Mkakati huu unamaanisha hakutokuwa na uboreshaji uwanja wa ndege na miundo mbinu ya utalii. Mkakati huu utapunguza magali ya madhara yajayo na uwanja wa ndege. Isipokuwa, utakuwa na athari mbaya kisera na kisiasa na kimaendeleo kwa ujumla. Kwani, kwa miaka mingi usafiri wa Mafia umekuwa ukitegemea boti za kienyeji zisizo na vigezo vya usalama, njia ya mzunguko kupitia Rufiji na Mkuranga; ndege ndogo zilizotua mara chache hasa wakati wa kiangazi kutokana na ubovu wa uwanja.

  Kuchukua mkakati huu ni kuendeleza umasikini Mafia na hisia ya wananchi kuwa serikali yao haiwajali. Lakini mkakati huu haumaanishi na kuhakikisha ya kuwa utazuia mmomonyoko wa maadili na uharibifu wa mazingira. Kwani, tayari kuna ishara kuwa maendeleo na athari mbaya hazikwepeki kwa vile wananchi husafiri maeneo mbali mbali na kuiga au kuleta mambo ya huko (video, madishi ya satelite, mavazi, n.k). Muhimu zaidi ni kuwa Mkakati huu utapingana na Sera ya MKUKUTA, Sera ya Utalii ya kufaidisha wananchi, ya MCC/MCA-T na makubaliano yake na Serikali ya Jamuhuri ya Tanzania. Hivyo, Mkakati huu hautokubalika na Siasa za Serikali ya Tanzania.

- **Mbadala wa kuwa na uingiaji wageni wengi Mafia**

  Huu unaweza kukuza uchumi kwa kuongeza kipato na uwanja wa ndege unaweza kuboreshwa sambamba na wingi wa wageni. Pia, itabidi kujenga hoteli na huduma nyingine za kukithi mahitaji ya wageni na katafuta vivutio zaidi kwa ajili ya utalii. Lakini bila ya kuwa na mpango kamambe wa uwiano wenye kuzingatia usimamizi bora wa mazingira na wa kisheria Mafia itaweza kupata mabadiliko mabaya na uharibifu mbaya wa kudumu usiorekebishika wa mazingira, maliasili na jamii. Haya yataweza kuzidisha badala ya kuondoa umasikini na kuboresha uchumi. Kupunguza wingi wa ujio wa wageni kidogo kidogo na kufikia idadi himilivu itakuwa mbinu na uamuzi/mkakati bora. Hata kama mkakati huu utapunguza mapato ya serikali, faida za uboreshaji mazingira zitakuja kuzaa matunda ya kipato bora baada ya muda mrefu wa utekelelezaji uhifadhi. Maamuzi makini yenye mantinki Ki-Sera yafanyike sasa kuchagua mkakati huu kwa kupima na kubaini faida na hasara ya kila mkakati mbadala husika kuupata ule mzuri na endelevu. Tayari MCC na Serikali wanajadili juu hili na kuna mpango kua idiadi ya wageni kwa situ itapingua hadi 40 kwa saa badala ya 100 kwa saa kama ilivyokusudiwa mwanzo. Mabadiliko haya hayataathiri michoro na mipango ya baadaye ya kukua kwa utalii kwa Mafiaa endapo dhana ya ukuaji wa uchumi itazingatiwa

- **Kuwa na watalii wachache wenye thamani kubwa**

  Ina maanisha kuwa na watalii wachache ambao watapunguza wageni kuwa wengi na kusababisha msongamano na uharibifu. Isipokuwa hao wachache ni wale watakaolipa pesa nyingi kutokana na shuguli zao. Hoteli na huduma za kitalii zitakuwa chache na bora sio ujezi mwingi wa hoteli. Mkakati huu unawiana na mkakati wa Taifa wa utalii wa kuwa na watalii wachache wa kutoa pesa nyingi. Kumudu mkakati huu budi kuboresha miundo mbinu ya utalii na kuwa na mpango wa watalii au wageni kujiandikisha na kuwahi nafasi (booking) za ujio wao Mafia kama njia ya kuzuia ujio mwingi holela wa watalii wengi kwa pesa kidogo. Pia muhimu ni kupanua vivutio anuai vya utalii wa wao kulipa pesa nyingi lakini wakaburudika kwa hali ya juu na kuutangaza utalii Mafia wakirudi kwao.

- **Kuboresha Hoteli zilizopo na kuzuia kujenga Hoteli mpya.**

  Kuna mpango wa kujenga hoteli zaidi 5 kuongeza 8 zilizokuwepo. Wawezezaji wamelenga fukwe zaidi na wengine wamelenga visiwa vidogo vidogo ambavyo ni maeneo ya mazalia ya viumbe vya bahari. Ili kupunguza madhara ya wingi wa hoteli, serikali inaweza kuweka mkakati na sera ya kuboresha na kupanua uwezo wa hoteli za kitalii zilizopo kwa kuweza kupokea watalii/wageni wengi zaidi kama mbinu mbadala ya kuepuka kujenga hoteli nyingi zaidi zitakazoathiri mazingira na maeneo tete ya mazalia ya kasa na viumbe vinginevyo vya bahari na nchi kavu. Upanuzi budi uzingatie vigezo vya kimataifa. Hii itasaidia pia kupunguza uchafuzi wa mazingira utokanao na maji taka na taka za mahoteli mengi; msuguano katika suala la ardhi itakayotakiwa na wawekezaji kutoka hasa miliki za mila; kuingilia maendeo ya uvuvi mdogo mdogo kwa shughuli za kitalii; usumbufu na shinikizo kwa ya maisha ya samaki mfano Potwe na wengineo.

  Kuboresha kwa kupanua vivutio ni gharama. Serikali ifikirie sera za motisha za kiuchumi ambazo zitawavutia wawekezaji katika sekta ya utalii kuboresha hoteli na huduma ili mazingira yawe bora na endelevu. Kuunganisha utalii wa Mafia na maeneo mengineyo ni mbinu mojawapo katika mkakati huu kuweza kukithi haja za watalii.

- **Kuboresha matumizi ya Nishaji Mbadala**

  Kuwa na nishati endelevu inayotegemewa inayopatikana wakati wote ni jambo muhimu katika maendeleo ya utalii wa Mafia. Serikali itaathirika kwa kukosa kodi na wananchi watakosa huduma na mapato. Kwa sasa, umeme wa Mafia hautabiliki kutokana na kukatika katika au kutokuwepo kila siku kutokana na ubovu/uzee wa genereta na mara nyingi kuisha nishati ya diseli ya kuendesha mitambo ya kuzalisha umeme.Kutokana na hayo hapo juu, ni muhimu kuamua ki-sera matumizi ya nishati mbadala ambayo ni endelevu ya kumudu gharama inayosaidia uwepo wa mazingira salama.

  Kuna nishati mbadala za aina mbili. Moja ni Nguvu ya Jua (Solar power) kama mbadala ila ya muda mfupi au ya nyongeza ikiwepo na ingine pale zinaposhindwa kuwepo. Solar inaweza kuzalishwa ndani ya Mafia ikalengwa kukidhi sekta muhimu (hoteli, uwanja wa ndege, ofisi, kaya). Hii itapunguza matumizi ya dizeli na matatizo ya uchakavyu/uharibifu wa mashine.

  Ya Pili ni waya ya umeme ya kupita chini ya bahari hadi Mafia (kutoka Dar es salaam, Kidatu, Songosongo n.k gridi za taifa) ambao utakuwa mkakati wa nishati wa muda mrefu. Hii itasaidia kuendesha viwanda, shughuli za ofisi, nyumbani na utalii na kuwezesha watu kujikimu na kuondoa umasikini. Hii itaendandana na sera ya nishati ya taifa ya kuufikisha umeme kwa wananchi ambayo ni nishati ya uhakika ya kuendesha viwanda. Manufaa ya mkakati huu ni mengi kimazingira, kijamii na kiuchumi isipokuwa gharama zake za kupitisha kebo baharini ni kubwa pamoja na kuweka uwiano kati ya upatikanai wa umeme na mikakati ya ulinzi wa vyazo vya maji, matumizi ardhi endelevu na ulizi wa mazingira.

HITIMISHO

Taarifa hii ya Mpango Mkakati wa mazingira kwa Mafia inonnesha kuwa uboreshaji wa uwanja wa ndege wa Mafia na shighuli nyingine zitakzotokana na ujenzi huo zitaleta faida na hasara kwa Mafia na taifa kwa ujumla.

Tathmini imeonesha kuwa Halmashauri ya Mafia haina uwezo wa kutosha wa kuandaa mipango ya uwiano wa maendeleo ya kisiwa na kuitekeleza kwa ufanisi kutokana na sababu zifuatazo:

- Upungufu wa watumishi na vitendea kazi (vifaa vya ofisi au vitendeakazi, usafiri)
- Uwezo mdogo wa kuwianisha, kuelekeza (mainstream) na kuratibu masuala ya mazingira katika mipango yote ya maendeleo ya Halmashauri pamoja na ya sasa pamoja na yajayo kama inavyoelekezwa katika Sheria ya Mazingira Na 191 ya 2004.
- Uwezo mdogo wa kuwianisha mipango yake na ya serikali kuu
- Umasikini walionao wananchi ambao ni sababu mojawapo kubwa ya matumizi yasiyo endelevu ya raslimali zilizopo hasa katika uvuvi na ardhi. Mahitaji ya samaki wengi kwa kipato imeleta uvuvi haramu na msuguano kati ya wananchi na wasimamizi wa hifadhi katika masuala ya uzingatiaji sheria. Hii inatokana pia na kuwa sekta nyingine za uchumi hazina ufanisi wa kutosha (kilimo, ufugaji, viwanda, biashara ndogo ndogo n.k). Vingine kama vile viwanda vya mbata vilivyokuwa vikitoa ajira miaka mingi iliyopita vimekufa na utalii ndio kwanza unaanza kukua.
- Utalii wa chini ya maji, wa mazingira na kiasi wa utamaduni unavutia watalii wengi kuja Mafia. Isipokuwa wananchi wengi hawajafaidika na utalii moja kwa moja na utalii huo (isipokuwa kwa kiasi kijiji cha Chole). Kutofaidika kukiendelea kunaweza kuathiri utalii suala la kuzingatiwa na halmashauri
- Uwezo mdogo wa kuhamasisha kila sekta iwafaidishe wananchi. Mfano ni sekta ya mifugo ambapo maziwa mengi hayapati soko na kumwagwa kutokana kuwa hakuna jinsi ya kuyahifadhi kwa matumizi ya ndani na kuyasafirisha kuyauza nje ya Mafia-Dar-es-salaam.
- Usimamizi mdogo wa masuala ya ardhi umesababisha baadhi ya wananchi kuuza ardhi kiholela kwa wawekezaji wa hoteli au wawekezaji kugawiwa ardhi rasmi jambo ambalo limezalisha malalamiko na kuhusisha viongozi na wasaidizi wao. Masuala ambayo yanahitaji kushughulikiwa ili kuwe na utalii endelevu

Taarifa hii ya Mkakati wa Mazingira wa Mafia inshauri kuwa kwa kuzingatia umuhimu wa mipango ya maendeleo na Mafia na mradi wa uboreshaji wa uwanja wa ndege na athari zake, Serikali Kuu na Serikali ya wilaya hazina budi kutoa kipaumbele na kutenga fedha kuetekeleza mapemdekezo yafuatayo.

MAPENDEKEZO

Na	Pendekezo	Maelezo
1	**Boresha Utawala Bora**	Hakikisha kuna ufanisi katika utekelezaji wa majukumu na usimamizi, uwajibikaji na ushirikishaji wananchi. Kuwe na uwazi katika maamuzi yanayozingatia sheria: • Anzisha/boresha katika Halmashauri ya Wilaya Ofisi ya Uratibu wa masuala ya Mazingira ili iweze kuingiza na kuwianisha masuala ya mazingira katika mipango yote ya maendeleo ya wilaya na ya serikali kuu inayotekelezwa wilayani • Tekeleza mpango wa kujenga uwezo wa Kamati tendaji za Halmashauri katika kuandaa, kusimamia na kutekeleza mipango ya uwiano ya maendeleo.

Na	Pendekezo	Maelezo
		• Boresha ushirikishaji wananchi katika maamuzi, kupanga na kutekeleza masuala yanayohusu maisha yao na shughuli za kujikimu • Kwa kushirikiana na AZISE mfano Haki Ardhi hamasisha na kuelimisha wananchi kuhusu sheria ya ardhi na jinsi gani wanaweza kutumianafasi zilizopo na zinazokuja kuboresha maisha yao. Saidia kuondoa vikwazo kijamii, ki-desturi, mifumo ya taasisi na mikakati na vikwazo vya fedha ili kufanikisha wa Mafia wawe na utayari na washiriki wao wenyewe ndani ya mchakato wa maendeleo yajayo.
2	**Panga Mpango Mpana wa Maendeleo Endelevu na wa muda mrefu**	Hakikisha kuwa kunapangwa mpango mpana (comprehensive) wa uwiano (integrated) ambao ni wa muda mrefu ambao utalenga maendeleo na ulinzi wa mazingira: **Tayarisha mpango wa matumizi ya ardhi unaoweka zone za matumizi borevu.** • Zingatia raslimali zilizopo na uhimilivu wa bioanua hizo • Anzisha Tume Maalum ya wataalamu wa ki-sheria kwa kuchunguza matatizo na malalamiko yaliyopo kwa sasa yahusuyo ardhi. Kisha, weka mwongozo wa kulinda maslahi na haki ardhi kwa wananchi na wawekezaji. Elekeza utendaji wa haki katika mapatano ya amali ya ardhi. • Toa mafunzo ya sheria ya ardhi kana inavyotakiwa na sheria hiyo na mifumo yake • Zuia kisheria ununuzi wa ardhi ufanyao na wawekezaji kutoka wamiliki wa ardhi ya kimila (wananchi) na kutoka serikalini. Wawekezaji wote wazingatie sheria ya uwekezaji ya kupata ardhi kutoka TIC (Kituo cha uwekezaji). • Zuia/kataza na elimisha wananchi wasiuze ardhi bali waingie ubia wa haki na wawekezaji kwa kuzingatia sera ya MKURABITA • Unda mfumo wa kunufaisha wananchi kutokana na uwekezaji pamoja na utalii kisiwani wapate haki ya mafao. Mfumo wa kufaidika na utalii unotumika Chole unaweza kuboreshwa ili utumike katika maeneo mengine Mafia ili kuondoa umasikini. Mfumo huo utasaidia wananchi kutokuuza ardhi kwa kificho na kukubali kuwekeza katika ubia ili wanufaike.
		Wizara ya Mali ya Asili na Utalii na Halmashauri ya Mafia itayarishe Mpango wa Utalii endelevu Hakikisha ya kuwa mpango wa utalii endelevu unazingatia uhimilivu wa kisiwa katika kubeba mzigo wa utalii unaotarajiwa, Mpango uliopo wa Uwiano wa Usimamizi wa Raslimali za Pwani na Mpango wa Taifa wa Utalii. Mpango budi: • Uwe na malengo, viashiria na viwango na ufafanue aina ya utalii na maeneo gani yatahusika; uonyeshe jinsi utakawianishwa na maendeleo ya wilaya kwa ujumla ili mapato yaboreshe maendeleo yake • Mpango utoe mwongozo kwa wawekezaji katika utalii kuwa wanatakiwa kufanya nini na wasifanye nini katika shughuli hizo mbali mbali za utalii na kuhakikisha kuwa wanazingatia • Mpango utambue na kuonyesha mahitaji ya sekta ya utalii na kuhakikisha yanapatikana au kufanikishwa. Mfano mahitaji ya huduma mbali mbali, wahudumu kujua kuongea kiingereza na lugha nyingine muhimu mfano Kifaransa, Kiitaliano, Kiswahili fasaha na kuhakikisha kuwa kunajengwa Chuo cha Mafunzo cha kukithi mahitaji hayo na kuwa vyuo binafsi vinaelekeza mitaala katika kukidhi mahitaji ya mafunzo ya stadi za kazi katika sekta husika za Mafia (languages, tour guide, hotel management, housekeeping, food & bevarages, languages, boat rides & repair services). • Kutoa mwongozo kwa wawekezaji, vyombo vya usafiri (boti, ndege nk.) katika sekta ya utalii kuhusu idadi ya watalii inayoruhusiwa kwa msimu/mwaka, inayoruhusiwa kutembelea eneo fulani au kufanya shughuli fulani ya utalii kwa siku, aina ya utalii unaokaribishwa, idadi na aina ya majengo ya hoteli na ukubwa wake ili kupunguza shinikizo haribifu kwa kisiwa kidogo chenye ukomo fulani wa kubeba mzigo. Kila kitu duniani kina ukomo wake wa kupokea kuelemewa.

Na	Pendekezo	Maelezo
		Wizara ya Miundombinu kwa Kushirikiana na Mamlaka ya Bandari na Halmashauri ya Mafuia itengeneze mpango kamambe wa ujenzi wa Gati Wananchi walio wengi wanategemea usafiri wa bahari ambao kwa sasa hutumia gati ya Kilindoni Mafia, Mkuranga, Rufiji na Kilwa (Kisiju, Nyamisati n.k). Mpango wa kuboresha gati ya Kilindoni umekwisha kukamilika. Kutokana na historia ya kijamii, uchangianji raslimali na maeneo ya uvuvi, mawasiliano ya jamii kati ya Zanzibar, Mafia, Rufiji, Mkuranga na Kilwa; kuwepo kwa ukuaji utalii kanda ya kusini (Mafia, Kilwa, Selou-Rufiji) ni vizuri mpango wa uboreshaji gati wa maeneo yaliyotajwa hasa Rufiji, Kilwa, Mkuranga yakaoanishwa kwa manufaa ya wilaya hizi zote kwani kila moja imekutwa ina mipango ya gati, kuboresha uchumi na utalii.
		Halmashauri Iboreshe Mpango mkakati wa utupaji taka maji na taka ngumu • Mpango utenge eneo la utupaji taka ngumu na utoe maelekezo jinsi kutekeleza mpango na shughuli za utupaji taka pamoja na mfumo wa motisha kwa wale watakaopunguza uchafuzi wa mazingira • Kuhamasisha wananchi katika kuelewa madhara na kuzingatia misingi salama ya utupaji taka katika vifao wanavyomudu na usimamizi shirikishi wa usafi wa mazingira • Halmashauri kutumia nyenzo za tathimini ya Mazingira pamoja na tathimini ya miradi katika athari zake katika uchafuzi na uharibifu wa mazingira na maisha ya watu kwa miradi yote itakayoanzishwa. Kujenga uwezo wa watumishi wa halmashauri kutahitajika ili hili litekelezwe kikamilifu • Kutekeleza miradi ya vyoo bora, usafi wa mazingira na kuwa na mkakati wa kuzoa taka ambazo zitatupwa na kutendewa (waste management) kuzingatia sheria na viwango vilivyowekwa kitaifa na kimataifa. Halmashauri inaweza kutoa mkataba kwa kampuni au AZISE kusimamia suala na utupaji takamaji na taka ngumu pamoja na kinyesi na kuona kuwa hakuna utupaji hovyo katika mazingira (ardhi, bahari, mito)
3	**Chukua hatua ya kushughulikia Athari za Mazingira**	**Upatikanaji wa Maji** • Wizara ya Maji na Miundombinu ya Umwagiliaji pamoja na Halmashauri ya Mafia ifanye utafiti wa maji ya ardhini kujua kiasi kilichopo na utoshelevu wake kwa matumizi mbali mbali kabla ya kuruhusu uanzishaji mkubwa wa hoteli, viwanda n.k • Kuwataka wawekezaji wa viwanda, hoteli, kutumia teknolojia sanifu ya maji inayopunguza upotevu wa maji na kuwataka wawekeze katika vyanzo mbadala vya maji (mfano ya mvua) a mbayo yatapunguza tegemezi ya maji ya ardhi. • Kutumia sheria ya ulipaji kwa kiasi cha maji yanayotumiwa na kutumia mapato katika kuboresha miundombinu husika ya maji (mapato ya maji yaboreshe mfumo wa maji) • Kuhakikisha ya kuwa maji salama yanawafikia wananchi na kutoa kipaumbele kwa wale waishio katika visiwa vidogo nje ya kisiwa kikubwa cha Mafia na kuwa miundombinu yao ya uvunaji maji inaboreshwa • Wizara ya Mali asili na Utalii kuona kuwa inaweka
		Mahitaji ya Nishati • Wizara ya Mali Asili ya Utalii iwatake wawekezaji wapya katika sekta ya utalii kukithi angalau asilimia 50% ya mahitaji yao ya nishati kutoka bionuai mbadala za nishati (mionzi ya jua, upepo). • Hazina itoe motisha ya mapungufu ya kodi kwa wawekezaji watakaokidhi mahitaji yao ya nishati kutokana na teknolojia salama na borefu ya mazingira ambayo itapunguzia serikali mzigo wa kuwapatia nishati ya umeme kutoka gridi ya taifa. Halmashauri inaratibu waanzilishi hao na kuihakikishia Hazina kuhusu wawekezaji hao. • Wizara ya Nishati na Madini iangalie na kutoa kipaumbele cha kuipatia mafia umeme kutoka gridi ya Taifa kupitia kebo salama za chini ya bahari.

Na	Pendekezo	Maelezo
4	**Kutengeneza mkakati wa kuboresha maendeleo kiuchumi**	Ili wananchi wa mafia na wilaya ifainike kiuchumi na maendeleo yajayo yafuatayo yanasisitizwa: • Halmashauri na TANROAD na Wizara ya Miundombinu kuhakikisha barabara za ndani kubwa na ndogo zinaboreshwa na kuunganishwa na kuboresha usafiri wa bahari kuiunganisha Mafia na Bara • Kuhamasisha wananchi watumie nafasi zilizopo na zitazo za uchumi na kuboresha shughuli zao katika sekta zao husika kwa manufaa yao • Halmashauri na Wizara ya Elimu kuhakikisha ya kuwa wanajenga na kukisimamia Chuo cha Mafunzo ambacho mtaala wake utakidhi mahitaji ya stadi za kazi zinazohitajika Mafia kukidhi suala ya wananchi kupata ajira na kujiajiri wenyewe katika miradi mbali mbali. • Halmashauri na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko kuhamashisha kiwanda/viwanda vya mchakatuo wa mazao ya kilimo ambavyo vitatoa ajira na kuboresha kipato (wananchi wameomba kurejeshwa kiwanda cha zao la minazi). • Halmashauri ikishirikiana na Bank ifanikishe mikopo nafuu kwa ajili ya wajasiriamali ambao nao wapate mafunzo ya kujua wajibu wao katika mikopo na maendeleo yao. Kutoa kipaumbele kwa vijana na akinamama.
5	**Chukua Hatua ya Pupunguza Makali ya Athari katika Jamii**	Ili kupunguza athari mbaya ya maendeleo kwa jamii yafuatayo yazingatiwe: • Kuwaelimisha wananchi kuhusu madhara ya utalii katika mila na desturi. • Kwa kushirikiana na Wizara ya Utalii, Halmashauri itunge mwongozo wa kuwafahamisha watalii desturi zitakiwazo kuzingatiwa wafikapo na wawapo Mafia na kufuatilia kuhakikisha kuwa hoteli za kitalii na watalii wanazingatia hayo • Halmashauri ifanikishe kujengwa kwa shule za kutosheleza za sekondari ambazo zitakuwa kamilifu katika vifaa vya kisasa (pamoja na computer), walimu na kuhakikisha kuwa watoto wa kike na wakiume wanasoma na kumaliza masomo. • Halmashauri ishirikiane na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kuona kuwa kunapatikana boti ambayo itatumika kama ambulensi ya kusaidia kusafirisha wagonjwa wa dharura hasa akina mama wajawazito wenye matatizo ya kujifungua. • Vilevile Halmashauri na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii iwezeshe AZISE na Idara husika za Wilaya utekelezaji wa kuzuia maambukizi ya Ukimwi kama sera na mkakati wa kutokomeza Ukimwi unavyoelekeza. Kuwa na mipango kamambe ya kuelimisha wananchi kwa undani jinsi mmaambukizi yanavyowezekana na isivyowezekana; kuwahamasisha kupima katika vituo mbadala, kuwapatia taarifa wanazohitaji, kutokomeza nyanyapaa, kusaidia waathirika na yatima na kuzingatia miiko ya kazi. • Ofisi ya Waziri Mkuu Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ihakikishe kuwa Idara za Halmashauri zina wafanyakazi wanaotakiwa kama kasma inavyosema na kwa ujuzi unaotakiwa. Hawa wawe na vitendea kazi na usafiri ili waweze kuwa na ufanisi na kukidhi mategemeo na utoaji huduma unaotegemewa.

Utekelezaji wa ushauri huu unaweza kuanza mara moja kama raslimali (fedha, vifaa, watumishi) vinapatikana mara moja. Utayarishaji wa mipango iliyotajwa katika taarifa hii nayo inaweza ikaanza mara moja wakati uwanja wa ndege unaendelea kujengwa mradi tu madhara na mikakati borefu iliyotajwa katika tathimini ya mazingira ya uwanja wa ndege na huu Mkakati wa Mazingira wa Mafia itazingatiwa ili kuleta ufanisi katika utekelezaji kwa muda mfupi iwezekanavyo.